

HALMASHAURI YA MJI WA KASULU



Namba ya kotesheni: LGA/168/2022/2023/NC/01/L/02

Kwa ajili ya:

UTOAJI WA HUDUMA YA UWAKALA WA USAFI WA MAZINGIRA MJI WA KASULU KATIKA KATA ZA KUMSENGA, KUMNYIKA, MURUBONA, MURUSI, MWILAMVYA, KIGONDO, KIMOBWA NA NYANSHA

MWALIKO WA KOTESHENI

Tarehe 13 Juni, 2022

Halmashauri ya Mji KASULU inakusudia kutangaza kazi kwa ajili ya **UWAKALA WA USAFI WA MAZINGIRA MJI WA KASULU KATIKA KATA ZA KUMSENGA, KUMNYIKA, MURUBONA, MURUSI, MWILAMVYA, KIGONDO, KIMOBWA NA NYANSHA** Na inakusudia kutumia sehemu ya fedha kulipia malipo halali chini ya mkataba ambao unatolewa katika Mwaliko huu wa Kotesheni.

Unakaribishwa kuleta kotesheni yako ya bei kwa ajili ya utekelezaji wa kazi kama ilivyoelekezwa kwenye Maelekezo ya Mahitaji na bei kama ilivyofafanuliwa katika sehemu ya II.

Kotesheni zote ziwe na nakala halisi (original) nakala moja zinazofanana, zilizojazwa kwa usahihi na zilizowekwa kwenye bahasha isiyo na maandishi juu na kuandikwa "Kotesheni Na. **LGA/168/2022/2023/NC/01/L/02** Ni lazima kupelekwa kwa katibu wa Bodi ya zabuni ya Halmashauri ya Mji Kasulu, S.L.P 475 Kasulu ofisi ya kitengo cha ununuzi Ugavi, chumba Na.40 ghorofa ya pili.

Siku ya mwisho ya kuwasilisha kotesheni ni **Jumatatu tarehe 20 JUNI, 2022** kabla ya saa 4.30 asubuhi. Kotesheni zitafunguliwa hadharani mara tu baada ya ufunguzi, mbele ya wawakilishi wa wazabuni/mawakala watakao amua kuhudhuria katika ufunguaji wa zabuni katika ukumbi wa mikutano katika Halmashauri ya Mji Kasulu, S. L. P 475 Kasulu.

Kotesheni zitakazochelewa, sehemu ya kotesheni, kotesheni za kielektronik, na kotesheni zisizofunguliwa katika tukio la ufunguaji, kotesheni, kwa hali yoyote ile kotesheni hizo hazitakubaliwa kwa tathmini.

Na	Maelezo ya Zabuni	Kotesheni Namba
i	UTOAJI WA HUDUMA YA UWAKALA WA USAFI WA MAZINGIRA MJI WA KASULU KATIKA KATA ZA KUMSENGA, KUMNYIKA, MURUBONA, MURUSI, MWILAMVYA, KIGONDO, KIMOBWA NA NYANSHA	LGA/168/2022/2023/NC/01/L/02

Majukumu ya Wakala wa Usafi wa Mazingira.

- i. Kusafisha mifereji ya maji ya mvua na mitaro ya barabara katika maeneo wanayofanyia kazi.
- ii. Kuzoa taka kutoka kwa wazalishaji wa taka (maeneo ya makazi, sokoni na maeneo ya umma) na kuzipeleka eneo la dambo la Halmashauri.
- iii. Kusafirisha taka ngumu kutoka maeneo ya kuhifadhia taka kwa muda na kuzipeleka dambo kuu la Halmashauri.
- iv. Kutoza tozo za usafi kwa kutumia POS.
- v. Kuhakikisha kuwa taka zote zimeondolewa kwenye vizimba vya taka kwa wakati.
- vi. Kufanya usafi wa mazingira na kuzoa taka siku zote 7 za wiki.
- vii. Kuwa na vifaa vya kutosha na vinavyokidhi viwango kwa shughuli za usafi wa mazingira na uzoaji wa taka ikiwa ni pamoja na magari ya kubeba taka ngumu yasiyopungua 2.
- viii. Kuwa na nguvu kazi ya kutosheleza mahitaji ya kazi za usafi wa mazingira (kukusanya na kuzoa taka)

MASHARTI YA UJUMLA KWA WAOMBAJI

1. Mwombaji Lazima awe ni Raia wa Tanzania mwenye Umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea,
2. Mwombaji lazima awe na namba ya utambulisho ya Mlipa kodi (TIN Number) **(Hii itawahusu waombaji walio na mikataba ya GPSA ya kutoa huduma za usafi.**
3. Mwombaji lazima awe na akaunti ya Benki iliyo hai.
4. Mzabuni/Wakala lazima aambatanishe nakala yoyote kuonesha alikowahi kufanyia kazi kwa uzoefu zaidi.

UTAWALA
Halmashauri Ya Mji
KASULU

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MJI
KASULU